Nuru ya Kiswahili, Juzuu 4(2), Desemba 2025:74-102
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru42.74102

# Uchambuzi wa Matumizi ya Usimulizi kama Mbinu ya Kisanaa katika Vibonzo Jongevu vya Watoto

**Shadidu A. Ndossa**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha St. John's**
ashadidu@sjut.ac.tz

## Ikisiri

Makala hii inajadili mbinu mbalimbali za usimulizi zinazotumika katika vibonzo jongevu na sababu za kutumika kwake. Makala inabainisha kuwa watunzi hutumia mbinu zifuatazo za usimulizi: usimulizi wa moja kwa moja, usimulizi wa kuhamahama, usomaji wa kitabu, usimulizi wa ndotoni, pamoja na mbinu za kisasa kama usimulizi wa kiteknolojia na matumizi ya ujumbe mfupi. Aina hizi za usimulizi zinasaidia kuunganisha matukio, kusisitiza maudhui, ujenzi wa taharuki, kuhamasisha watoto kupenda kusoma, na kuendeleza utamaduni. Kupitia mifano mbalimbali kutoka katika vibonzo jongevu, makala imebainisha kuwa matumizi ya usimulizi katika vibonzo jongevu hutumika kufafanua hisia na matukio yasiyoelezwa na wahusika, kuunganisha na kusimamia mtiririko wa hadithi, kuelekeza tafsiri ya matukio kwa watazamaji, kutoa mtazamo mpana kwa kueleza hali na mawazo ya wahusika wote, pamoja na kuunda mtindo na utambulisho wa kipekee wa kazi husika. Data zilizozaa makala hii zimepatikana maktabani, ambapo mwandishi alitazama kazi mbalimbali za vibonzo jongevu na kuzifanyia uchambuzi kulingana na mahitaji yake. Nadharia ya Usimulizi wa Fasihi Simulizi imemwongoza mwandishi katika kukusanya na kuchambua data zake. Makala inahimiza ubunifu zaidi katika matumizi ya mbinu hizi kwa maendeleo ya watoto, hasa katika zama hizi za kidijiti ambapo teknolojia ni nyenzo muhimu ya uwasilishaji wa fasihi ya watoto.

**Dhana Muhimu**: usimulizi, mbinu ya kisanaa na vibonzo jongevu

## Utangulizi

Vibonzo jongevu ni michezo ya hadithi iliyotengenezwa kidijiti. Michezo hiyo huwasilishwa kama vipindi vya televisheni au kama vipande vya programu vinavyoweza kuwasilishwa kwa kutumia nyenzo na majukwa mbalimbali ya kidijiti. Kuna vibonzo jongevu kwa ajili ya hadhira maalum (kama vile watoto) na vingine kwa ajili ya hadhira yeyote. Makala hii inajadili vibonzo jongevu vilivyotengenezwa kwa ajili ya watoto. Vibonzo hivi huwa na wahusika wa kufurahisha na simulizi rahisi, mara nyingi hujumuisha funzo la maadili au elimu. Abdallah (2018) anaona kuwa, kimuundo, vibonzo jongevu vya watoto huwa na masimulizi mafupi mafupi ya dakika sita hadi kumi. Sifa zake nyingine ni: kuwa na maudhui ya kitoto; kutumia wahusika watoto; kuwa na matukio ya ufantasia; na mashindano au changamoto zinazowahamasisha kushirikiana na kufuata maadili mema. Vipengele hivi huundwa kwa uangalifu kulingana na umri na uelewa wa watoto, huku lengo kubwa likiwa kutoa elimu na burudani. Hivyo basi, katika makala hii, dhana ya vibonzo jongevu inatumiwa kurejelea vibonzo jongevu vya watoto.

Kwa kiasi kikubwa, vibonzo jongevu hutegemea lugha ya mazungumzo kama nyenzo kuu ya kuendeleza hadithi, ambapo wahusika hujibizana kwa lengo la kuwasilisha hisia, fikra, mitazamo na misimamo yao mbele ya hadhira inayokusudiwa. Mbali na mazungumzo ya wahusika, ushahidi unaonyesha kuwa usimulizi umekuwa ukitumika kwa ustadi mkubwa kama mbinu ya kisanaa katika vibonzo hivyo. Usimulizi, kama mbinu ya kisanaa, hurejelea kitendo cha kuelezea matukio, wahusika na mazingira kwa namna iliyo na mwanzo, kati na kikomo, ili kuvutia na kufundisha hadhira. Katika muktadha wa fasihi, usimulizi umetumika kama chombo cha kisanaa, burudani, mawasiliano na malezi ya kijamii, jambo linaloeleza kwa nini

mbinu hii imepata nafasi ya kipekee hata katika kazi za kifasihi za kisasa, ikiwemo vibonzo jongevu (Barthes, 1977).

Vibonzo jongevu kama kazi za kifasihi hujengwa kwa kuunganisha mbinu nyingi za kisanaa ili kuvutia na kuelimisha hadhira ya watoto. Watoto, kama hadhira kuu, huchochewa kupitia mazungumzo ya wahusika na simulizi linaloongoza matukio. Kupitia usimulizi, mtiririko wa hadithi huwekwa wazi, matukio hufungamanishwa, na wahusika hupata nafasi ya kuelezeka kwa kina ili kutoa mafunzo au falsafa za kijamii na kimaadili (Genette, 1980). Kwa namna hii, usimulizi unakamilisha pengo linaloweza kutokea endapo vibonzo jongevu vingetegemea mazungumzo pekee, kwani maelezo ya msimulizi hujenga daraja kati ya wahusika na hadhira. Hali hii huwasaidia watoto kuelewa maudhui ya vibonzo kwa urahisi zaidi na kuongeza mshikamano wa simulizi.

Matumizi ya usimulizi kama mbinu ya kisanaa katika vibonzo jongevu huchangia katika ujenzi wa muundo wa kazi na kuimarisha uwasilishaji wa mafunzo. Msimulizi huchukua nafasi ya kumwelekeza mtazamaji, kusisitiza mambo muhimu, na kutoa mwongozo wa kimaudhui. Mbinu hii huongeza mvuto wa kifasihi wa vibonzo jengevu na hutumika kama chombo cha kielimu na kijamii kwa kuwawezesha watoto kupata ujumbe mahsusi unaokusudiwa (Chatman, 1980). Pamoja na umuhimu huu wa usimulizi, bado umuhimu wake haujapewa nafasi kubwa katika maandiko ya kitaaluma. Hivyo basi, makala hii inajadili mbinu mbalimbali za usimulizi zinazotumika katika vibonzo jongevu.

## Kiunzi cha Nadharia

Makala imeongozwa na Nadharia ya Usimulizi wa Fasihi Simulizi. Huu ni mkabala wa kifasihi unaojikita katika kuchunguza kwa kina namna simulizi zinavyopangwa, kuwasilishwa, na kueleweka kwa hadhira. Inahusisha vipengele muhimu kama msimulizi, hadhira, wahusika, muda, mpangilio wa matukio, lugha, mitindo ya usimulizi, na mandhari. Lengo kuu la nadharia hii ni kuelezea mchakato wa uundaji wa hadithi na jinsi vipengele vyake vinavyosaidia kufikisha ujumbe kwa njia yenye mvuto na kuleta athari kwa wasikilizaji au watazamaji (Ong, 1982). Kwa kuzingatia nadharia hii, msanii wa kazi ya kisanaa hupata mwongozo wa kuchagua aina ya usimulizi, namna ya kuwasilisha wahusika, na jinsi ya kupanga matukio ili kusisimua au kuhamasisha hadhira (Finnegan, 1970).

Mwasisi wa nadharia hii ni Vladimir Propp ambaye alichambua muundo wa hadithi za kubuni za Warusi na kubaini kuwa zina vipengele vya msingi vinavyojirudia kama vile mhusika mkuu, mtoaji wa msaada, changamoto, na zawadi (Propp, 1968). Claude Lévi-Strauss naye alitazama hadithi kama mifumo ya kimaana inayodhihirisha fikra za msingi na mitazamo ya kijamii (Lévi-Strauss, 1978). Walter Ong alichangia kwa kuelezea tofauti kati ya usimulizi wa mdomo na maandishi, akionyesha kuwa usimulizi wa mdomo huwa na hulka ya kuwa wa kiutendaji, wa moja kwa moja na wenye ukaribu na hadhira (Ong, 1982). Ruth Finnegan alisisitiza umuhimu wa utendaji na mazingira halisi ya usimulizi wa fasihi simulizi barani Afrika, akionyesha kuwa usimulizi si matini tu bali tukio linaloishi kati ya msimulizi na wasikilizaji (Finnegan, 1970). Vilevile, Albert Lord na Milman Parry walichambua namna wahusika wa usimulizi wa kishairi wa mdomo walivyotumia mitindo ya kurudia na vina ili kujenga simulizi zinazokumbukwa kwa urahisi na kueleweka vyema.

Katika makala hii, Nadharia ya Usimulizi wa Fasihi Simulizi imesaidia kuchambua jinsi mbinu za usimulizi zinavyotumika katika vibonzo jongevu kama njia ya kisanaa ya kuwasilisha hadithi. Kwa kuzingatia misingi ya nadharia kama anavyobainisha Ong (1982), makala imeonyesha kuwa aina hizi za usimulizi huchangia kwa kiasi kikubwa kufikisha ujumbe kwa njia yenye mvuto, kueleweka kwa urahisi, na kuleta athari chanya kwa watazamaji wa vibonzo jongevu. Barber (2007) anaunga mkono hoja hii kwa kudai kuwa watunzi wa vibonzo jongevu hutumia mbinu mbalimbali za usimulizi kama usimulizi wa moja kwa moja, na kuhamahama kwa lengo la kuwasilisha simulizi kwa namna inayovutia, kueleweka kwa urahisi, na kufaa watoto au hadhira mahususi. Pia, Mitchell (1994) anaona kuwa Nadharia ya Usimulizi wa Fasihi Simulizi inaweza kutumika kuelewa jinsi usimulizi katika vibonzo jongevu unavyosaidia kushadidia maudhui, kunogesha simulizi, kuunga fasihi na nyuga nyingine na kuchochea fikra, hivyo kuwa nyenzo muhimu katika kuendeleza hadithi na urithi wa kijamii kwa namna ya kuvutia na yenye maana kwa kizazi cha sasa.

## Methodolojia

Data zilizozaa makala hii zimekusanywa kutoka maktabani, ambapo msisitizo uliwekwa katika kupitia na kuchambua vibonzo jongevu. Kwa mujibu wa Creswell & Creswell (2018), mbinu ya utafiti wa maktabani hutumika pale ambapo mtafiti anategemea vyanzo vya maandishi kama vitabu, makala, tasinifu, ripoti, na nyaraka nyinginezo zilizopo tayari, badala ya ukusanyaji wa data moja kwa moja kutoka kwa washiriki.

Mbinu iliyotumika kukusanyia data ni uchambuzi wa nyaraka laini, ambapo ulitumika mwongozo wa uchambuzi wa nyaraka hizo. Hii ilihusisha kuchambua yaliyomo katika kazi mbalimbali za kifasihi ambazo zilikuwa

na sifa ya kuwa na usimulizi wa hadithi. Mapitio haya yalihusisha kazi zaidi ya hamsini zilizochaguliwa kwa kutumia uchaguzi wa kimakusudi, ambapo vigezo vya msingi vilivyotumika ni kuwa kazi husika ziwe na maudhui ya usimulizi kama kipengele kikuu cha mawasilisho yake ya kisanaa. Uchambuzi wa nyaraka hizi ulilenga kubaini mbinu za usimulizi zilizotumika katika vibonzo jongevu na jinsi mbinu hizo zinavyosaidia kufikisha maudhui kwa hadhira mahsusi. Mogalakwe (2006) anaona kuwa mbinu ya utafiti wa maktabani huwa na manufaa makubwa katika tafiti za kifasihi kwa kuwa inamwezesha mtafiti kuoanisha maarifa ya awali yaliyopo na dhana au mitazamo mipya.

Makala imetumia muundo wa uchambuzi wa maudhui, ambapo mwandishi alitambua, kuchambua, na kufasiri namna usimulizi unavyojitokeza katika kazi husika (Bowen, 2009). Mbinu hii ni muhimu katika tafiti za kielimu na kijamii, kwani hutoa uelewa mpana wa yaliyomo katika nyaraka na namna yanavyohusiana na muktadha wa utafiti.

## Aina za Usimulizi Zinazotumika katika Vibonzo Jongevu

Katika sehemu hii, makala inaangazia aina mbalimbali za usimulizi zinazotumiwa na watunzi wa vibonzo jongevu pamoja na sababu za matumizi hayo. Aina za usimulizi zinazowasilishwa ni saba. Nazo ni: usimulizi wa moja kwa moja, usimulizi wa kuhamahama, usimulizi wa kusoma kitabu, usimulizi wa ndotoni, usimulizi wa kiteknolojia, usimulizi wa vikaragosi, na usimulizi wa kusoma ujumbe mfupi. Aina hizi zinajadiliwa katika kurasa zinazofuata:

**Usimulizi wa moja kwa moja**

Katika aina hii ya usimulizi, msimulizi anashika nafasi ya msingi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi. Ingawa yanakuwapo mazungumzo kati ya wahusika, mazungumzo hayo huwa machache mno. Mfano wa wazi wa matumizi ya usimulizi wa aina hii unaweza kuonekana katika kazi nyingi za *Swahili Fairy Tales*, ambazo, kwa kiwango kikubwa, humtumia msimulizi na kuwapa wahusika nafasi ndogo ya majibizano. Mifano ya kazi zenye mtindo huu ni pamoja na "Mfalme Mwenye Madevu", "Ndoto ya Mkama Maziwa", "Alice Kwenye Nchi ya Ajabu", "Mfalme Chura", "Jini Ndani ya Chupa", na "Rapunzel in Swahili". Vilevile, baadhi ya kazi za *Clangers* na *Sarah and Duck* zinatumia mbinu ya usimulizi wa moja kwa moja. Kwa mfano, katika hadithi ya "Mfalme Mwenye Madevu" inaanza kwa sauti ya msimulizi ikisema:

> **Msimulizi**: *Hapo zama za kale palikuwepo ufalme mkuu uliotawaliwa na Mfalme Mkubwa. Mfalme alikuwa na binti mrembo aliyetarajia kumuoza. Japokuwa binti huyu alikuwa mrembo, alijawa na majivuno pamoja na kiburi moyoni. Alijiona mzuri kupita kiasi na kuwadharau wote waliokuja kutaka kumuoa. Kila aliyeletwa kwake alikemewa, mwingine alisemwa ana pua ndefu, mwingine kifua chake kimechoka, mwingine anatembea kama bata, na mwingine ana sauti mbaya kama korongo. Hakuna aliyeonekana kumfaa.*
>
> *Wazazi wake walijitahidi kumshawishi awe na adabu na kuwaheshimu watu, lakini binti huyo aliendelea na dharau zake. Siku moja, mfalme alikasirika sana baada ya kuona mwanaume mwingine ametukanwa mbele ya hadhara. Kwa hasira, aliamua kumpa binti huyo kwa mwanaume wa kwanza atakayebisha hodi kwenye lango la kasri, iwe*

> *ni masikini, mchoraji, au muuza kuni. Na kweli, hakuchelewa—muda si muda, kijana maskini aliyekuwa mpiga kinubi alipita akitaka msaada. Mara moja, mfalme alimteua kuwa mume wa binti yake. Kwa binti huyo ilikuwa kama ndoto mbaya, lakini hakuwa na la kufanya. Aliagizwa kufunga mizigo yake na kuondoka na mumewe kwenda kuanza maisha mapya ya unyenyekevu na kazi ngumu* (Chanzo: https://www.youtube.com/watch?v=r02PLAt_pYQ 2025)

Katika dondoo hili, msimulizi anashikilia nafasi ya msingi katika kuendesha simulizi zima. Yeye ndiye anayeelezea kila kitu, kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi, hali inayoonesha wazi kuwa mbinu hii imetokana na fasihi simulizi, ambako fanani ndiye aliyekuwa na mamlaka ya kusimulia, kueleza, na hata kuongoza hisia za hadhira. Msimulizi ndiye anayeanzisha hadithi kwa mtindo wa kimapokeo kama vile "Hapo zama za kale...", akitoa muktadha wa awali wa matukio na kumtambulisha msikilizaji kwenye mazingira ya kifalme pamoja na wahusika wakuu. Anaendelea kueleza tabia ya binti wa mfalme, migogoro inayotokea, maamuzi ya mfalme, na hata matokeo ya maamuzi hayo. Mohamed (1995) na Mulokozi (1996) wanaona kuwa matumizi ya msimulizi hufanya kazi kama mwongoza hadithi, mwalimu wa maadili, na mfasiri wa matukio

Licha ya kusimulia, msimulizi pia anatumia kiimbo cha sauti kupanda na kushuka ili kuwasilisha hisia mbalimbali kama vile furaha, mshangao, huzuni au hasira. Kwa mfano, anapotaja majivuno ya binti au hasira ya mfalme, sauti yake hubeba uzito unaofaa, jambo linalomfanya msikilizaji ambaye ni mtoto aweze kuelewa kwa kina hisia zinazotawala katika tukio husika. Hili linaongeza uhai na mvuto wa hadithi, likimwezesha mtoto

kusikia, kuelewa na kupokea ujumbe wa hadithi kwa njia ya kufurahisha na inayoeleweka kirahisi. Kwa mujibu wa Mohamed (1995) na Finnegan (2012), matumizi ya kiimbo ni mbinu ya kisanaa yenye mizizi katika fasihi simulizi ambayo lengo lake ni kuonesha hisia za msimulizi. Pia, husaidia sana kuongeza umakini wa hadhira.

Pia, ili kuipa hadithi uhalisi na mvuto zaidi, msimulizi huingiza majibizano machache baina ya wahusika, hasa katika sehemu muhimu kama vile maamuzi ya kifalme au majibu ya binti kwa wachumba waliomfuata. Ingawa ni msimulizi anayesimulia sehemu kubwa ya hadithi, majibizano haya husaidia kuonesha hisia za moja kwa moja za wahusika na hivyo kuongeza uhalisia wa simulizi na kulifanya livutie zaidi. Kwa jicho la kinadharia (kuhusu nafasi ya msimulizi), msimulizi katika hadithi hii anachukua nafasi ya uongozi wa kimahadhi kwa kusimulia, kufasiri, na kuathiri hisia za msikilizaji kwa njia inayotokana moja kwa moja na mbinu za fasihi simulizi. Bakize (2014) anaona kuwa uchanganyaji huu huifanya hadithi iwe hai, ya kueleweka, na yenye kufundisha, mambo ambayo ni muhimu sana katika fasihi ya watoto.

**Usimulizi wa kuhamahama**

Kwa mujibu wa Abdallah (2018), usimulizi wa kuhamahama ni ule unaojitokeza kwa vipindi maalumu katika kazi ya kifasihi. Hii ina maana kwamba msimulizi huchagua baadhi ya matukio muhimu kuyasimulia, huku akiyaacha mengine yaelezwe kupitia mazungumzo ya wahusika au kuachwa kabisa bila simulizi. Mara nyingi, msimulizi huyatumia maelezo yake kufafanua matendo au muktadha unaohusiana na wahusika ili kusaidia watazamaji kuelewa kwa undani kilicho mbele yao. Kwa mfano, katika *Ubongo Kids* (2021) msimulizi anasema yafuatayo:

**Msimulizi**: *(Huku wakianza kuosha vyombo) Akili alimsaidia baba kuosha vyombo. Ili kuufanya uoshaji vyombo uwe wa kufurahisha, Akili na baba wanaigiza kila chombo kama mtoto anayehitaji kuogeshwa. Walimpa kila mmoja jina na kuwaimbia wimbo wakati wa kuwaogesha.*

**Akili**: (Huku akiosha vyombo na kuimba) *lalalalaa laala lalalaaa.*

**Msimulizi**: (*Akili anaonekana akiwa amelala kitandani*) *Usafi umemalizika na muda wa kulala sasa. Usiku mwema Akili. Ndoto njema Akili. Oooh! Upo Lala Land Akili. Sijui ni nini?*

**Happy Hippo**: (Huku akimgusa Akili*) Tap, find you. It's your time* (Nimekugusa, ni zamu yako sasa).

**Msimulizi**: (*Huku Akili akionekana kushangaa*) *Ooh! Rafiki zako wanacheza mchezo wa kidali na Happy Hippo amekushika wewe. Kimbia Akili unatakiwa kumshika mwingine.*

**Akili**: (Huku akimkimbiza Little Lion) *Touch you Little Lion. Hahahaa hahaaa!*

**Msimulizi**: (*Huku Little Lion akianza kuwakimbiza wenzake*) ***Sasa ni zamu ya Little Lion. Sijui mara hii atamshika nani jamani?*** (Chanzo: Ubongo Kids, 2021).

Katika dondoo hili, mtunzi anaonesha namna msimulizi anavyofanya kazi yake kwa kuhamahama mara tatu. Lengo ni kumsaidia mtoto ambaye ni hadhira kuelewa kile anachokiona katika vibonzo jongevu. Mtunzi ametuwekea matukio yanayofuatana kwa haraka sana. Katika tukio la kwanza, tunamuona Akili akiwa anamsaidia baba kuosha vyombo. Kisha, anaoneshwa Akili akiwa amelala kitandani; na baadaye, anaoneshwa Akili akiwa anacheza mchezo wa kidali na rafiki zake. Ingawa wahusika wanazungumza, msimulizi anatumika kwa lengo la kuonesha uhusiano wa

matukio yote matatu ili mtazamaji asipotee. Pia, katika mfano huu, msimulizi anatumika kufanya ufafanuzi. Kwa mfano, katika tukio la mwisho ambapo Akili anaonekana kushangaa, msimulizi anamfafanulia mtazamaji mambo mawili. Kwanza, huo ni mchezo wa kidali; na, pili, kwa kuwa Akili ameshaguswa na mwenzake, itakuwa jukumu lake sasa kuanza kumsaka mtu.

Utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Basque (UPV/EHU) mwaka 2019 unaonyesha kuwa vibonzo jongevu vyenye muundo wa masimulizi (kama vile mbinu ya utangulizi-kiini-suluhu) unawasaidia watoto kuelewa vizuri mtiririko wa hadithi na maadili yaliyofunzwa. Aidha, muundo wa masimulizi humpa msikilizaji nafasi ya kujenga muunganiko wa matukio na kuelewa maana yote kwa urahisi, ikilinganishwa na zile zisizo na mpangilio uliobainika za "mtindo usio wa kisimulizi", yaani ambazo zinawakosesha watoto kuelewa sababu na matokeo ya matukio ya hadithi.

**Usimulizi wa kusoma kitabu**

Mbinu ya usimulizi wa kusoma kitabu, kama ilivyoelezwa na Abdallah (2018), ni njia mpya na ya kipekee inayojitokeza mara chache katika vibonzo jongevu. Mbinu hii hutumia kusoma kwa sauti sehemu zilizochaguliwa za kitabu cha hadithi kwa lengo la kuimarisha na kunogesha simulizi kuu. Sehemu hizi za kitabu huchaguliwa kwa uangalifu, mara nyingi ni kurasa chache tu, ambazo huambatana na picha zinazoeleza kwa undani yaliyomo, ili kusaidia hadhira, hasa watoto, kuelewa vizuri na kwa urahisi ujumbe unaotolewa. Katika CBeebies (2020) kuna mfano ufuatao:

> **Dog**: (*Huku wakiwa wanaangalia kitabu kikubwa cha zamani*) *This is a book by my granny Pog and*

*it is called Granny Bug's Guide to Ancient Egypt.*

**Msimulizi**: (*Dog na rafiki yake, huku wakiwa wanaingia ndani ya kitabu*) *Welcome fellow explorers we're about to go on a journey back in time 5000 years before you were born and the whole world was a beach. This isn't a beach and the old world was a sandpit when this part of the world was a desert and still is today look dog a pyramid, I think.*

**Tafsiri**

**Dog:** (*Wakiwa wanaangalia kitabu kikubwa cha zamani*)

"Hiki ni kitabu cha bibi yangu Pog, kinaitwa Mwongozo wa Bibi Bug Kuhusu Misri ya Kale".

**Msimulizi:** (*Dog na rafiki yake wanapoingia ndani ya kitabu*)

*"Karibuni wajasiri wa safari! Tuko karibu kuanza safari ya kurudi nyuma kwa muda wa miaka 5000 kabla ya kuzaliwa kwenu, wakati dunia yote ilikuwa ufukwe wa bahari. Hapa si ufukwe! Dunia ya zamani ilikuwa kama kisima cha mchanga - sehemu hii ya dunia ilikuwa jangwa, na bado ni jangwa hadi leo. Tazama Dog - piramidi, nafikiri!* (Chanzo: CBeebies, 2020).

Kwa kutazama dondoo hili, ni wazi kuwa mbinu ya usimulizi kwa kutumia kitabu inatoa msisimko wa kipekee katika uwasilishaji wa hadithi kwa sababu huunganisha simulizi la mdomo na maelezo ya kuona kupitia picha za kitabu. Hii huwafanya watoto kuwa na uzoefu wa kipekee wa kusikia na kuona hadithi kwa wakati mmoja, jambo linaloimarisha kumbukumbu na uelewa wa maudhui. Aidha, usomaji huu wa kitabu unakuwa sehemu ya simulizi kamili, ambapo msimulizi hutumia lugha ya kueleweka, toni zinazovutia, na wakati mwingine huongeza maelezo ya ziada yanayoelezea hisia, mazingira au tabia za wahusika, ili kuwafikia watoto kwa ufanisi

zaidi. Matumizi ya kitabu kama sehemu ya usimulizi yanaendana na msingi wa Nadharia ya Usimulizi wa Fasihi Simulizi ambapo Finnegan (1970) anaona kuwa ni jukumu la mtunzi 'kuisoma' hadhira na kujua mahitaji yake. Kwa kuwa walengwa wa vibonzo jongevu ni watoto, matumizi ya mbinu ya usomaji kitabu huwa mwafaka kwa kuwa huu ndio wakati sahihi wa kujenga misingi ya usomaji vitabu.

Mbinu ya kusoma kitabu inasaidia kuimarisha uhusiano wa mtoto na hadithi. Pia, huwahamasisha watoto kupenda kusoma vitabu. Hivyo, husaidia na kuchangia kukuza utamaduni wa usomaji kutoka umri mdogo. Hii ni kwa sababu watoto wanapojifunza kuona vitabu kama sehemu ya burudani na si kazi ngumu, hujitahidi kuwa na hamu ya kujifunza na kusoma wenyewe. Wapo wataalamu mbalimbali wa lugha na maendeleo ya watoto wanaoona kuwa uchanganyaji wa masimulizi ya mdomo na usomaji wa vitabu una mchango mkubwa katika kukuza lugha, fikra, na uelewa wa watoto. Kwa mfano, Isbell, Sobol, Lindauer, na Lowrance (2004) wanaona kuwa watoto wanaoshiriki katika simulizi yenye kuchanganya usomaji wa vitabu huonesha maendeleo makubwa zaidi katika matumizi ya lugha ngumu/tata na uelewa wa muundo wa hadithi ikilinganishwa na wale wanaosimuliwa bila kuchanganya. Utafiti wao unaonyesha kuwa kuunganisha hadithi za mdomo na maandishi kunawasaidia watoto kuongeza msamiati, kufikiria kwa undani, na kushiriki kikamilifu katika mawasiliano.

Vilevile, tafiti kama za De Agosto (2016) na Grolig (2020) zinaunga mkono hoja hii kwa kubainisha kuwa watoto wanaojifunza kupitia hadithi wanakuwa na msingi imara wa uelewa wa lugha ya maandishi kwa kuwa simulizi huambatana na mpangilio wa matukio, matumizi ya lugha ya hisia

na matendo, na mwingiliano wa kihisia kati ya msomaji na hadhira. Katika muktadha wa Kiafrika, ambapo utamaduni wa simulizi za jadi ni imara, kuunganisha mbinu hii na usomaji wa vitabu kunaweza kuimarisha usomaji na uandishi miongoni mwa watoto, hasa katika mazingira yenye changamoto za vitendea kazi au elimu ya awali. Uchanganyaji huu huongeza ushiriki wa watoto, huwafanya kuwa wasikilizaji na wasimuliaji bora, na huwajengea msingi wa ustadi wa kusoma na kuandika ambao ni muhimu kwa mafanikio ya kielimu.

Pia, katika Storytime *with Nana*, msimulizi husoma hadithi kwa utulivu huku akionyesha picha za kurasa mbalimbali za kitabu. Katika *Reading Rainbow*, msomaji hutumia vitabu mbalimbali na kuunganisha maelezo na picha kwa ajili ya kuvutia watoto. Abdallah (2018) anaongeza mifano mingine kutoka katika vibonzo kama vile *Peppa Pig* na *Akili and Me*. Anasema kuwa huonyesha sehemu za msomaji kusoma hadithi au kuelezea kurasa za vitabu. Pia, huunganisha simulizi hilo na mazungumzo ya wahusika ili kuhakikisha hadhira inafuatilia kwa urahisi na kufurahia.

**Usimulizi wa ndotoni**

Usimulizi wa ndotoni hujulikana pia kama usimulizi wa kimawazo. Hii ni mbinu ya kisanaa inayojitokeza pale ambapo simulizi linafanyika ndani ya fikra au ndoto ya mhusika. Katika aina hii ya usimulizi, tukio husimuliwa si katika hali halisi ya uhusika bali kama sehemu ya kile anachokiwaza au kukiota mhusika. Kwa kawaida, mhusika haonekani akizungumza moja kwa moja, bali sauti ya msimulizi husikika ikifafanua kile kinachotokea ndani ya ndoto au fikra zake. Mara nyingi, sauti hii hujifananisha na sauti ya ndani, ambayo huendana na hali ya utulivu au mazingara yasiyo ya kawaida yanayoendana na ulimwengu wa ndoto au fikra. Mbinu hii huleta

mguso wa kihisia na mshikamano wa kiakili kati ya hadhira na mhusika. Aidha, ni mbinu inayowezesha kufichua undani wa wahusika, hasa matarajio, hofu, matamanio au mawazo yao ya ndani ambayo hayawezi kueleweka kirahisi kupitia mazungumzo ya kawaida.

Kwa, mfano, mhusika Kibena katika *Akili and Me*, mara nyingi, huonyeshwa akielekea mahali pa ndoto panapoitwa '*Lala Land'*. Hapa, matukio yote ya ndotoni yanasimuliwa kwa kutumia sauti ya msimulizi badala ya Kibena mwenyewe kuyasimulia au kushiriki kama katika ulimwengu wa kawaida. Kibena anapoingia *Lala Land*, husikika sauti ya msimulizi ikielezea kile anachokiona au kupitia. Jambo hili linaonekana katika mfano ufuatao:

> **Msimulizi**: *Kibena alipofumba macho na kulala, alijikuta katika ulimwengu wa ajabu wenye rangi ang'avu, miti inayoongea na wanyama wanaoimba. Alipowasogelea, mmoja wao alimkaribisha kwa furaha*... (Chanzo: Ubongo Kids, 2021).

Katika dondoo hili, hadhira husafiri pamoja na Kibena katika ulimwengu wa mawazo au ndoto, huku msimulizi akielezea matukio hayo kwa utulivu na mwonekano wa kifasihi. Mbinu hii huongeza mvuto wa kisanaa na hufungua fursa ya kuingiza maadili, mafundisho au changamoto zinazoweza kueleweka kwa njia rahisi na ya kufurahisha.

Pia, katika *Blue's Clues*, mbinu ya usimulizi wa kimawazo hutumika mara kwa mara. Mhusika mkuu (Josh) huingia kwenye dimbwi la fikra zake ambapo kile anachowaza husimuliwa kwa sauti ya ndani au picha zinazofuatilia mtiririko wa mawazo hayo. Hapa, hadhira huwekwa ndani ya

akili ya mhusika ili kuona anachowaza kabla hajafanya uamuzi au kuelewa jambo fulani kama inavyooneshwa katika dondoo lifuatalo:

> **Msimulizi**: (*Huku Josh akiwa ameshika kidevu na kuzama katika dimbwi la mawazo*) *Hmm… Steve anajiuliza, Je, Blue anataka kucheza mchezo mpya? Anafikiria kuhusu ishara zote tatu, na ghafla picha ya mchezo wa kuficha inamjia akilini…* (Chanzo: Nickelodeon, 2025).

Katika mfano huu, tunashuhudia sauti ya ndani ya mhusika ikielezea mchakato wa kufikiri, huku picha zikionyesha kile kinachoendelea ndani ya fikra. Mtindo huu huimarisha uhusiano kati ya mtoto na mhusika, huku ukitilia mkazo fikra bunifu, uchambuzi wa kihisia, na maamuzi ya kibunifu. Kwa ujumla, mbinu ya usimulizi wa ndotoni au wa kimawazo hutoa fursa ya pekee katika kazi za vibonzo jongevu kwa kutoa uwanja mpana wa ubunifu na uwasilishaji wa maudhui kwa njia ya ndani na ya kuvutia. Kwa watoto, mbinu hii husaidia kujenga uwezo wa kuelewa hali ya ndani ya mhusika, kuchochea fikra za kufikiri kwa undani, na kukuza mazoea ya kutafakari kabla ya kutenda.



Picha ikimwonesha mhusika wa *Blue Clues* akiwa anafikiria vifaa vya muziki atakavyotumia, ambapo mara nyingi kile anachofikiri huwasilishwa kwa hadhira kwa kumtumia msimulizi (Chanzo: Nickelodeon).

Mbinu hii ya kisanaa inaonekana kama sehemu muhimu ya vibonzo jongevu, ambapo mhusika anaongea au kufikiri ndani ya nafsi yake (kimya), lakini hadhira husikia mawazo hayo kupitia sauti ya msimulizi. Mbali na kutoa ufahamu wa ndani wa mhusika, mbinu hii hulifanya simulizi kuwa na uzito wa kihisia na uhalisia zaidi, kuongeza ufantasia na kuongeza mvuto kwa hadhira. Keymer (2020) anadai kwamba mbinu hii inaruhusu mawazo, hisia, na mitazamo ya mhusika kuunganishwa kikamilifu na sauti ya msimulizi bila kutumia nukuu au viashiria kama "alisema" au "alifikiri". Aidha, Gingerich (2013) anabainisha kuwa mbinu hii inasafirisha mawasiliano ya ndani ya mhusika si kwa maneno ya sauti tu bali kupitia sauti ya msimulizi, hivyo inaongeza urahisi wa hadithi kwa msikilizaji.

**Usimulizi wa kiteknolojia**

Usimulizi wa kiteknolojia ni mbinu ya kisanaa inayojitokeza pale ambapo vifaa vya teknolojia vinatumika kama njia au nyenzo ya kuwasilisha au kusukuma mbele simulizi katika kazi ya kifasihi ya watoto, hususan katika vibonzo jongevu. Mbinu hii hujumuisha matumizi ya vifaa kama vile simu janja, televisheni, kompyuta, kishikwambi, kamera za usalama (CCTV), au hata roboti zenye uwezo wa kuwasiliana na binadamu. Vifaa hivi vinaweza kuwa wahusika wenyewe au visaidizi vya simulizi vinavyosaidia kutoa taarifa, kufichua siri, au kuhamasisha mabadiliko ya kiuhusika au kimaudhui.

Tofauti na mbinu nyingine za simulizi zinazotegemea zaidi mazungumzo au sauti ya msimulizi wa kawaida, usimulizi wa kiteknolojia hutegemea kifaa cha kidijiti (*digital interface*) kuwasilisha taarifa au kufanya mwendelezo wa simulizi. Abdallah (2018) anaona kuwa mbinu hii inaendana na mahitaji ya kizazi cha sasa cha watoto wanaokua katika mazingira yaliyojaa teknolojia. Abdallah (ameshatajwa) anaendelea kudai kuwa athari chanya ya teknolojia inaonekana kila pahala iwe katika taa za barabarani, benki, shuleni, msikitini, kanisani, na hospitalini. Hivyo, matumizi ya vifaa vya kidijiti katika masimulizi ni mwendelezo wa kile kilichowazunguka watoto na hivyo kuwawezesha kuelewa na kufurahia maudhui kwa urahisi. Kwa mfano, katika kipindi cha *Akili and Me*, Kibena mara nyingi huiambia hadhira: "*Hebu tuone kwenye kompyuta kinachoendelea*!" Baada ya hapo, hadhira hupelekwa kutazama televisheni ambapo huwekwa video zinazohusiana na hadithi ya siku hiyo.

Mbinu hii inatambuliwa na wataalamu wa fasihi ya watoto kama chombo cha kisasa kinachoboresha stadi za kusikiliza, kuangalia, na kuchambua

maarifa yanayotolewa kupitia vyombo vya kidijiti. Utafiti wa Hughes & John (2020) unaonesha kuwa teknolojia ya kuona na kusikia kama televisheni, kishikwambi na programu bunifu huongeza ushiriki wa watoto katika hadithi na kuwasaidia kuunganisha maarifa mapya na hali halisi ya maisha yao ya kila siku. Hali hii huonesha jinsi vifaa vya kiteknolojia vinavyoweza kutumika kama sauti ya pili ya msimulizi, kwa kusaidia kuelekeza hadithi, kutoa nyongeza ya kimaudhui, au kutoa maarifa mapya kwa njia ya burudani. Hivyo basi, usimulizi wa kiteknolojia ni mbinu ya kisanaa na wakati huohuo hutumika kama nyenzo ya kujifunzia, inayoakisi mabadiliko ya kijamii na kiutamaduni yanayoendelea katika karne ya 21.

**Usimulizi wa vikaragosi**

Hii ni mbinu ya kisanaa ya kusimulia inayochanganya wahusika halisi na wa kubuniwa mfano wa mdoli au mwanasesere. Usimulizi huu umekuwa na mchango mkubwa katika fasihi ya watoto, hasa kupitia vipindi vya televisheni vinavyowavutia watoto. Vikaragosi hivi vinaweza kuwa vya kidijiti, vya mikono (au vya kutengenezwa kwa vifaa mbalimbali) na hutumika kama wasimulizi wa kazi husika, wakiwa na sauti, tabia, na hulka zinazowavutia watoto. Tofauti na simulizi za kawaida, vikaragosi husimulia kwa kuzungumza moja kwa moja na watazamaji, kufafanua matukio, kuibua hisia, au kutoa mawaidha kwa njia ya burudani.

Jurkowski (2023) anadai kuwa vikaragosi vinapotumika vema sambamba na usimulizi wa hadithi huwafanya watoto wajihusishe zaidi na simulizi kwa sababu ya sura za kirafiki, sauti za kuchekesha na lugha rahisi inayotumika. Hii ina maana kwamba matumizi ya vikaragosi huongeza ladha na kuifanya hadithi kuwa na mvuto zaidi. Kwa mfano, katika kipindi cha *Mr. Maker*, vikaragosi wa Shapes huibuka katikati ya kipindi na kutoa

changamoto kwa watazamaji. Mara nyingi, husikika mhusika Mr. Maker akisema "Sasa ni zamu ya SHAPES kutafuta nani ataweza kutengeneza kitu cha kipekee kwa kutumia mstatili! Hebu tuone!" Hali kama hiyo hujitokeza pia katika *Justine's House* ambapo Justine Clarke huwasiliana na vikaragosi kama Little Monster, Mimsy na Fluff ili kusimulia masimulizi kuhusu maadili ya kila siku kama vile urafiki na usafi wa mwili. Kipindi maarufu cha *Sesame Street* hutumia mbinu hii kupitia wahusika kama Elmo na Cookie Monster ambao hutoa masimulizi ya kijamii, kitaaluma na kitabia kwa njia ya kuchekesha na inayovutia watoto (Abdallah, 2020). Fisher (2020) na Bakize (2018) wanaongeza kuwa mbinu hii imechotwa katika fasihi ya kijadi (fasihi simulizi). Wanasema kuwa mbinu hii ya usimulizi kwa kutumia vikaragosi imechotwa huko kwa kuwa watunzi wanaamini kuwa huongeza mvuto wa kisanaa na huimarisha uelewa wa watoto kuhusu ujumbe wa kazi ya fasihi.



Picha ya kikaragosi *Little Monster* kinachotumika katika kibonzo jongevu cha *Justine House* (Chanzo: CBeebies, 2023)

Matumizi ya vikaragosi kama chombo cha masimulizi ni mbinu ya zamani iliyokuwa na nafasi ya pekee katika burudani na elimu ya watoto. Katika tamthilia ya *Punch and Judy*, iliyotokea Uingereza katika karne ya 17, msimuliaji mmoja alicheza nafasi zote kwa kutumia vikaragosi vya glavu (*glove puppets*) na kubadilisha sauti kila alipokuwa akimwakilisha mhusika tofauti (Fisher, ameshatajwa). Hali hii iliwawezesha watazamaji, hasa watoto, kutofautisha wahusika kwa sauti, lafudhi, na mitindo ya mazungumzo. Bascandziev (2022) anaongeza kuwa matumizi ya vikaragosi

katika masimulizi ya watoto hayajaanza sasa bali yana umri mrefu. Anadai kuwa katika vipindi vya kizamani vya televisheni kama *Howdy Doody* na kazi za *Marionette Theatre*, vikaragosi vilitumika kuwasilisha maadili, mafunzo na burudani, huku sauti za wahusika zikitolewa na msimulizi au msanii mmoja au wawili waliobobea katika mbinu ya kubadilisha sauti. Hii inaonyesha kuwa mbinu ya kutumia vikaragosi si mpya, bali ni urithi wa kisanaa ulioendelea kwa sura tofauti hadi kufikia vibonzo jongevu. Hii inamaanisha kuwa matumizi ya vikaragosi yamechotwa katika fasihi simulizi na kusasishwa ili yalingane na muktadha wa sasa wa kidijiti. Mbinu hii inawiana na yale aliyopendekeza Ong (1982) katika Nadharia ya Usimulizi wa Fasihi Simulizi, ambapo inasisitiza kuhusu matumizi ya mbinu za kifasihi simulizi inayoendana na muktadha na mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia.

**Usimulizi wa kusoma ujumbe mfupi**

Mbinu ya kisanaa ya usimulizi kupitia kusoma ujumbe mfupi imekuwa kipengele muhimu katika vibonzo jongevu vinavyolenga watoto. Hii ni mbinu ambayo huanzisha au kuendeleza simulizi kwa kupitia mawasiliano yaliyoandikwa, ambayo husomwa na mhusika mkuu kwa namna ya kuvutia na inayojumuisha watazamaji. Katika kipindi cha *Mr. Maker*, mhusika mkuu hupokea ujumbe wa mara kwa mara kutoka kwa watoto walioko katika maeneo mbalimbali duniani wakimwalika kuja kushiriki katika shughuli za kisanaa katika mazingira yao. Ujumbe huwa na maudhui yanayohusiana na mada ya siku hiyo, na huanzisha sehemu muhimu ya simulizi ambapo Mr. Maker hufanya ziara na kuonyesha watoto jinsi ya kutengeneza kazi za sanaa kwa kutumia vifaa rahisi. Ong (1982) anaona kuwa mawasiliano baina ya fanani na hadhira ni jambo muhimu na husaidia kunogesha simulizi. Maelezo ya Ong (ameshatajwa) yanawiana na

msimamo wa Finnegan (1970) kupitia Nadharia ya Usimulizi wa Fasihi Simulizi ambapo anasisitiza kuhusu kuwapo kwa mawasiliano baina ya fanani na hadhira.

Kwa kuangalia matumizi ya ujumbe mbalimbali unaotumwa kwa Mr. Maker, ni wazi zimekuwa sehemu muhimu ya simulizi zake na huchangia hadhira kuelewa masimulizi yake. Pia, kuna matumizi ya kimakusudi ya teknolojia kuwasilisha ujumbe, ambapo mara zote Mr. Maker hupokea ujumbe mfupi kwenye kifaa kinachofanana na kishikwambi. Anapoufungua ujumbe huwa katika hali ya maandishi au video, ambapo moja kwa moja ujumbe huo huchukua nafasi ya msimulizi na kuendeleza simulizi. Buckingham (2015) anaona kuwa uchanganyaji wa teknolojia na masimulizi halisi huwafanya watazamaji, hasa watoto, wajihusishe moja kwa moja na mchakato wa hadithi kwa kuhusisha teknolojia na masimulizi ya ubunifu. Anaongeza kuwa mbinu hii inachochea uelewa wa watoto kuhusu matumizi ya teknolojia kama chombo cha mawasiliano na mafunzo, jambo linaloendana na mwelekeo wa elimu ya kisasa unaosisitiza uwasilishaji wa kidijiti katika fasihi ya watoto. Hali kama hiyo hujitokeza pia katika vibonzo jongevu vya *Blue's Clues*, ambapo mhusika Blue hupokea ujumbe kutoka kwa watazamaji. Mathalani, katika *Blue's Clues* kuna mfano ufuatao*:*

**Joe**: (*Akiwa amesimama mbele ya Mailbox*) *We just got a letter. We just got a letter. We just got a letter. We just got a letter. Wonder who it's from*.
(*Anafungua ujumbe*).
**Joe**: Oh! look. It's a letter from our friends.
**Ujumbe wa 1 (*Boy*)**: (*Huku Joe akiwa anasoma*):
"**Hi, Steve. I help with dinner because I'm able… place mats out on the table**.

**Ujumbe wa 2 (*Girl*)**: (*Huku Joe akiwa anaendelea kusoma ujumbe wa pili*): "***I sort the laundry, socks by two… it's a job that I can* do**" (Chanzo: CBeebies, 2024).

**Tafsiri**

**Joe:** (*Amesimama mbele ya Sanduku la Barua*) *Tumepata barua. Tumepata barua. Tumepata barua. Tumepata barua. Najiuliza imetoka kwa nani*.
(*Anafungua ujumbe*).
Joe: *Oooh! Tazama*. *Ni barua kutoka kwa marafiki zetu*.

**Ujumbe wa 1 (Mvulana):** (*Joe akisoma*): "***Habari, Steve. Nasaidia maandalizi ya chakula cha jioni kwa sababu ninaweza… kuweka mikeka mezani***."

**Ujumbe wa 2 (Msichana):** (*Joe akiendelea kusoma ujumbe wa pili*): "**Napanga nguo za kufua, soksi mbili kwa mbili… ni kazi ambayo naweza kufanya**." (Chanzo: CBeebies, 2024).

Kwa kuangalia dondoo hapo juu, ni wazi kuwa usomaji wa ujumbe umetumika kama sehemu ya kuendeleza simulizi za Blue Clues. Ujumbe wa kwanza unaelezea shauku ya mhusika kuhusu kupata chakula cha usiku na ujumbe wa pili unaelezea kuhusu kufua soksi. Masimulizi kwa njia ya ujumbe huwanufaisha watoto kwa njia mbalimbali. Kwanza, hujifunza umuhimu wa mawasiliano ya maandishi, kuandika na kusoma ujumbe kwa umakini. Pili, huwachochea kuwa wabunifu na washiriki hai, kwani ujumbe huwa na wito wa moja kwa moja wa kushiriki kwenye shughuli au kutatua matatizo yanayojitokeza katika simulizi. Ngugi (2010) anaongeza kuwa aina hii ya usimulizi huimarisha uhusiano baina ya wahusika na hadhira kwa kuunda mazingira ya ushiriki wa kihisia na kielimu. Aidha, Ngugi

(2011) anaongeza kuwa mbinu shirikishi zinapotumika katika kazi za watoto kama vitabu, maigizo, nyimbo na mashairi huchangia kukuza ujuzi wa lugha, kuendeleza stadi za kijamii, na kufundisha maadili kwa njia ya mawasiliano yenye heshima na shauku.

## Hitimisho

Mbinu za usimulizi katika vibonzo jongevu zinachangia kwa kiasi kikubwa kufanikisha malengo ya elimu, burudani, na malezi kwa watoto. Kupitia usimulizi wa moja kwa moja, usimulizi wa kuhamahama, usomaji wa kitabu, usimulizi wa ndotoni, usimulizi wa kiteknolojia, na vikaragosi, vibonzo hivi huweza kuwafikia watoto kwa njia rahisi, ya kuvutia, na yenye maudhui yenye tija. Mbinu hizi zinasaidia kuunganisha matukio, kusisitiza maudhui muhimu, kuendeleza utamaduni, na kuwahamasisha watoto kupenda kusoma na kujifunza. Kwa kuwa hadhira ni watoto, mbinu hizi zinapaswa kuendelezwa kwa ubunifu zaidi ili kuhakikisha watoto wanapata masimulizi yenye maana, yanayovutia na yanayowasaidia kukuza fikra, hisia, na utamaduni wao. Hivyo, usimulizi katika vibonzo jongevu ni njia ya kuwasilisha hadithi na hutumika kama daraja muhimu la kukuza elimu, maadili, na utamaduni miongoni mwa watoto.

## Marejeleo

Abdallah, S. (2018). *Nafasi ya fasihi ya watoto ya kidijiti katika kukuza fasihi simulizi: Mifano kutoka katika vibonzo jongevu* (Tasnifu ya uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Abdallah, S. (2020). Uhusika wa kitoto katika vibonzo jongevu: Mbinu ya kisanaa ya kuivuta hadhira ya watoto. *Mwanga wa Lugha*, 5(1), 75-86. Moi University Press.

Bakize, L.H. (2014). *Utangulizi wa fasihi ya watoto*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.

Bakize, L.H. (2018). Mbinu ya kuvuta makini ya watoto katika fasihi ya watoto. Katika M. Kandagor & M. Mukuthuria (Wah.), *Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na maendeleo yake* (uk. 13-25). Dar es Salaam: TATAKI.

Barber, K. (2007). *The anthropology of texts, persons and publics: Oral and written culture in Africa and beyond*. Cambridge: Cambridge University Press.

Barthes, R. (1977). *Image, Music, Text*. London: Fontana Press.

Bascandziev, I., & Harris, P. L. (2022). Preschoolers' gesturing when playing with puppets versus watching puppets. *Early Childhood Research Quarterly, 60*, 148-160. https://doi.org/10.1016/j.ecresq.2022.03.003*Bluey* (2018-). *Baby Race* [Season 2, Episode 49]. Bluey TV. Retrieved on January 26, 2026, from https://www.bluey.tv/watch/season-2/baby-race/

Bowen, G.A. (2009). Document analysis as a qualitative research method. *Qualitative Research Journal, 9*(2), 27-40.

Buckingham, D. (2015). *The media education manifesto*. Cambridge, UK: Polity Press.

Chatman, S. (1980). *Story and discourse: Narrative structure in fiction and film*. Ithaca, NY: Cornell University Press.

Creswell, J.W., & Creswell, J.D. (2018). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (5th ed.). Thousand Oaks, CA: Sage.

De Agosto, D.E. (2016). Unveiling the literacy benefits of storytelling. *Children and Libraries, 14*(2), 3-6. https://journals.ala.org/index.php/cal/article/view/5990

*Dog Loves Books: Dog Loves Pyramids* [TV episode]. (2020). Katika *Dog Loves Books* (Season 1, Episode 26). BBC / CBeebies.

*Dora the Explorer* (2000-2019). *Boots' Special Day* [Season 3, Episode 13]. Dora Fandom. Retrieved January 26, 2026, from https://dora.fandom.com/wiki/Boots%27_Special_Day

Finnegan, R. (1970). *Oral literature in Africa*. Oxford: Oxford University Press.

Finnegan, R. (2012). *Oral literature in Africa*. Cambridge: Open Book Publishers. https://doi.org/10.11647/OBP.0025

Fisher, J.R. (2020). *Puppetry and early childhood learning: How stories come alive through characters*. New York: Little Lantern Media.

Genette, G. (1980). *Narrative discourse: An essay in method* (J. E. Lewin, Trans.). Ithaca, NY: Cornell University Press.

Gingerich, J. (2013). The benefits of free indirect discourse. *LitReactor*. https://litreactor.com/columns/the-benefits-of-free-indirect-discourse

Grolig, L. (2020). Shared storybook reading and oral language development: A bioecological perspective. *Frontiers in Psychology, 11*, Article 1818. https://doi.org/10.3389/fpsyg.2020.01818

Hughes, J., & John, A. (2020). *Digital storytelling in early childhood: Creative engagement and multimodal narratives*. London: Routledge.

Isbell, R.T., Sobol, J., Lindauer, L., & Lowrance, A. (2004). The effects of storytelling and story reading on the oral language complexity and story comprehension of young children. *Early Childhood Education Journal*, 32(3), 157-163.

Jurkowski, S. (2023). Puppets as a pedagogical tool in early childhood education. *Education Sciences, 13*(3), 291. https://doi.org/10.3390/educsci13030291

Keymer, T. (2020). *Free indirect discourse in Jane Austen: Writing, society, politics*. Oxford: Oxford University Press.

Lévi-Strauss, C. (1978). *Myth and meaning*. New York: Schocken Books.

Lord, A.B. (1960). *The singer of tales*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Mfalme mwenye madevu|King Grisly Beard in Swahili | Hadithi za Kiswahili [Video]. (n.d.). YouTube. Imechukuliwa Julai 30, 2025, kutoka YouTube.

Mitchell, W.J.T. (1994). *Picture theory: Essays on verbal and visual representation*. Chicago: University of Chicago Press.

Mogalakwe, M. (2006). The use of documentary research methods in social research. *African Sociological Review*, *10*(1), 221-230.

Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za nadhari ya Kiswahili: Riwaya, tamthiliya na hadithi fupi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mulokozi, M.M. (1996). *Oral literature: The African experience*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Nickelodeon (2025, July 20). *Blue's Clues & You!* [YouTube channel]. YouTube. https://www.youtube.com/@bluesclues

Ngugi, P.M.Y. (2010). Nafasi ya ubunifu katika michezo ya watoto wa 'Mchongoano'. *Kioo cha Lugha, 8*, 67-89.

Ngugi, P.M.Y. (2011). Ufundishaji wa fasihi ya watoto katika shule za msingi nchini Kenya. *Kioo cha Lugha, 9*, 84-89.

Ngugi, P.M.Y., Lyimo, E. B., & Bakize, L. H. (2014). *Fasihi ya Kiswahili ya watoto: Maendeleo, nadharia, mbinu na mifano ya uchambuzi*. Dar es Salaam: TUKI.

Ong, W.J. (1982). *Orality and literacy: The technologizing of the word*. London: Methuen.

*Peppa Pig* (2004-). *Muddy Puddles* [Season 1, Episode 1]. Peppa Pig Fandom. Retrieved January 26, 2026, from https://peppapig.fandom.com/wiki/Muddy_Puddles_%28episode%29

Propp, V. (1968). *Morphology of the folktale* (L. Scott, Trans.). Austin: University of Texas Press. (Kazi asilia ilichapishwa 1928)

The Adventures of Abney & Teal (2023). *The Adventures of Abney & Teal S01E01 The Porridge Party* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=uBd_TDkGOmg&list=PLsaWct-i1S0cuUUyDyVd0EOv9bnuzraak

*Thomas & Friends* (1984-). *Trouble in the Shed*. Ttte Fandom. Retrieved January 26, 2026, from https://ttte.fandom.com/wiki/List_of_Thomas_%26_Friends_episodes

Ubongo Kids. (2021). *Vikombe vya Lala Land: Jifunze Kiingereza na akili, katuni za elimu kwa watoto* [Video]. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=LbhfSDQWExs

UNIMA. (n.d.). Punch and Judy. In *World Encyclopedia of Puppetry Arts*. Imechukuliwa Julai 30, 2025, kutoka https://wepa.unima.org/en/punch-and-judy/